

## Kadi ya burudani/michezo

Kila mtu kati ya miaka 6 na 18 anapata Kadi ya Burudani/michezo ya kroner 1000! Kadi ya burudani/michezo ni kadi ya zawadi unayoweza kutumia kwa shughuli za kupumzika za kawaida.

Lillehammer itaruhusiwa kuwa manispa/comune, ya majaribio ya Kadi ya Burudani/michezo. Mpango wa serikali ni kwamba hii iwe ofa ya kitaifa, ya kudumu. Lillehammer ni miongoni mwa manispaa/comune ambazo zitajaribu jinsi mpango kama huo unaweza kupangwa na ni changamoto gani zinapaswa kutatuliwa njiani. Hatujui kitakachotokea baada ya kipindi chetu cha majaribio, lakini tunafurahi kwa fursa ambazo watoto wa Lillehammer wanapata wakati wa kipindi cha majaribio.

Kadi ya burudani/michezo ni kwa kila mtu kabisa katika kikundi cha umri sahihi. Mnamo Agosti 2021, kila mtoto aliyezaliwa kati ya mwaka wa 2003 na mwaka wa 2015 wanapata 1000 krona kulipia shughuli za kupumzika/michezo ya kawaida. Katika maandalizi, kila mtu katika umri unaofaa atapata kadi mpya ya zawadi

ya 1000 krona . Ikiwa shughuli inagharimu zaidi, tumia Kadi ya Burudani/michezo ya sehemu ya gharama na uongeze mwenyewe pesa ambayo itakuwa imezidi. Pesa haziwezi kutumiwa kwa matumizi mengine, haziwezi kulipwa moja kwa moja kwa familia, haziwezi kuwekwa kwa kipindi fulani kwenda kwenye kipindi kingine ,na huwezi kutumia kwa ndugu wengine. Kila mtoto wa umri sahihi anapata Kadi yake ya Burudani/michezo.

Nenda kwenye [lillehammer.aktiv-fritid.no](http://lillehammer.aktiv-fritid.no) ili uone ni nini unaweza kutumia Kadi yako ya Burudani/michezo! Hapa ndipo unaweza kuona ni pesa ngapi kwenye Kadi ya Burudani/michezo ya mtoto, na wakati umepokea facture ya shughuli za kupumzika, iliyoandaliwa, unaweza kuilipa ukitumia Kadi hiyo ya Burudani ikiwa shirika limechagua kushiriki katika mradi/mpango huo. Je! Shughuli yako haimo kwenye orodha/liste? Waulize na uwasiliana na [fritidskortet@lillehammer.kommune.no](mailto:fritidskortet@lillehammer.kommune.no) ili ujiunge na mradi/mpango wa burudani/michezo.

Unapojiandikisha, lazima uchague Kinorweyi kama lugha yako - lakini wakati umesajiliwa/umeandikwa na umeingia, unaweza kubadilisha lugha mufano Nynorsk, Kiingereza, Somali au Kiarabu. Labda inaweza kuwa kama sehemu itatafsiriwa katika lugha zaidi mwishowe. Katika mipangilio, unaweza pia kuchagua "maandishi kamili" au "maandishi rahisi ya kusoma", na uchague kuona alama zinazoonyesha yaliyomo katika kila shughuli. Habari ambayo mashirika tofauti huingia kwenye muhtasari bado iko katika Kinorwe.

Soma zaidi kuhusu mwongozo kwenye [www.lillehammer.kommune.no/fritidskortet](http://www.lillehammer.kommune.no/fritidskortet).



LILLEHAMMER  
KOMMUNE